# LBE 2009 – Migration

# Episode 7:

# The Football Player

**Author: Mouhamadou Awal**
**Editor : Thomas Mösch**
**Translator: Anne Thomas**

---

**Characters:**
**Narrator:**
**Voiceover:**
**Félix,** male (29)
**Fariqou Oumarou,** young male

---

## Introduction

Hujambo na karibu kwenye sehemu nyingine katika mfululizo wa makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji kati ya Afrika na Ulaya. Leo tunaanza kwa kutafakari juu ya waafrika ambao wamerudi makwao baada ya kuishi hapa Ulaya kwa miaka kadhaa. Je wamepata ufanisi gani? Maisha yao yako vipi baada ya kurudi nyumbani Afrika? Wanaeleza vipi kuhusu maisha yao walipokuwa Ulaya?. Hebu kwanza tukutane na kijana ambaye alikwenda Ulaya kwa ajili ya kucheza mpira wa kulipwa. Spoti hasa mpira ni fani inayowavutia vijana wengi kutoka Afrika. Wanaona kuwa wacheza mpira wanaojulikana wanatengeneza fedha nyingi huku Ulaya na nchi za Amerika. Hzeina Félix kutoka Cameroon anatueleza kuwa, sio rahisi kupata mafanikio ya kuwa mchezaji mpira wa kulipwa katika nchi za nje. Baada ya yote hayo alifanikiwa kuanzisha kampuni yake mara tu aliporudi nyumbani – anataka kuwa mfano wa kuigwa na vijana wa Cameroon watakaopenda kuzifuata nyayo zake.

**1. Atmo_garage of Hzeina and Sons**

**2. Voice clip Félix_1**

Jina langu ni Hzeina Félix. Nilicheza mpira kwenye timu ya daraja la kwanza nyumbani Cameroon. Nilishiriki kwenye mashindano ya kombe la LG huko Iran. Halafu nilikaa msimu wote China mpaka baadaye nilipokwenda Ulaya. Na sasa nimerudi nyumbani Cameroon, tena kwenye kweye mkoa nilikozaliwa wa – Adamaoua. Nimeanzisha biashara ya nyumba na viwanja pamoja na biashara ya usafirishaji. Nadhani ninaweza kutoa huduma nzuri ya teksi kwa watu na familia . Watoto wanapenda sana mpira kwa hivyo mimi hutoa huduma ya kuwasafirisha katika maeneo ambayo huwa wanakwenda kutahiniwa kwa ajili ya klabu za mpira.

**3. Atmo : fade out to young footballers training in the background**

**4. Narrator:**

Hzeina Félix ana miaka 29. Angalau mara moja kwa wiki, anahudhuria mazoezi katika klabu mbalimbali huko Ngaoundéré mji ambao ndio uliomfungulia yeye milango ya kutoka, na huko yeye hutoa mawaidha kwa wachezaji chipukizi. Yeye alikuwa anacheza nafasi ya mshambuliaji katika timu ya Pyunik FC Yerevan huko Armenia, sehemu inayopakana na Uturuki. Lakini alilazimika kuacha kucheza kwa sababu ya kuumia. Aliamua kuwasaidia kifedha wachezaji mpira chipukizi, na pia kutumia fedha zingine kuanzisha biashara hiyo ya . nyumba na usafirishaji kwa ajili ya kutoa ajira kwa vijana nyumbani kwao. Hafahamu lolote kuhusu mahesabu na usimamiaji wa biashara kwa hivyo ameajiri watu wa kufanya kazi hiyo.

**5. Voice clip Félix_2**

Ninafuatilia biashara yangu kwa kando. Kuna watu wachache ambao wanasimaia mali zangu. Wananifahamisha kila kinachoendelea kwa simu. Hatusiti kufanya maamuzi kwa sababu lazima tuongeze pato letu ambalo tumelipata kwa taabu. Kwa hivyo tunafunga mikanda. Wao wanafaidika kutokana na fedha zangu kama vile mimi ninavyofaidika kutokana na kazi yao.

**6. Atmo_phone reception** *(from archive)*

7. **Narrator:**

Hzeina and Sons ndio kampuni pekee inayotoa huduma za magari ya kukodi katika mji wa Ngaoundéré. Kuna zaidi ya magari 60 katika uwanja wa kuegeshea magari. Kampuni hiyo imewaajiri wafanyakazi 100 kuna wasimamizi wa mahesabu, wafanyakazi wa gereji na madereva. Wafanyakazi hao hubadilishana zamu asubuhi na mapema jioni. Mwanzoni Felix alipata tabau…

**8. Voice clip Félix_3**

Ni vigumu kwa sababu wacheza kandanda ambao wamefikia kiwango fulani wanaona vigumu kubadili na kuanza kufanya kazi nyingine. Ni sawa na mtu anaetaka kugeza mbingu kuwa ardhi. Lakini tunajua kuwa pindi mwili ukikataa basi hapo lazima ubadili, ufanye kitu kingine ambacho kiwe kinakaribiana na kandanda. Hatuwezi kuacha mpira na kuwa wajenzi kwa mfano. Ingawa ni rahisi kwa vijana ambao bado hawajaingia ndani sana katika mpira. Wanachohitaji ni kufanya maamuzi mazuri…

**9. Atmo_ young footballers training**

**Music**

**10. Narrator:**

Félix anafikiri kwamba kufanikisha matarajio yake ni lazima abadilishane mawazo na wachezaji mpira chipukizi na mameneja wa kampuni yake. Hutumia muda wa kutosha kukagua viwanja mbali mbali katika mji wa Ngaoundéré na pia kutafuta vipaji. Hasiti katika swala la kuendeleza vipaji vya wachezaji chipukizi. Anaeleza anachokifanya:

**11. Voice clip Félix_4**

Katika kiwango hiki tunamwangalia kila mtu – tunaangalia mambo yote mawili afya na uwezo wa mtu. Tunatazama jinsi wanavyoumudu mpira kwa sababu wengine wanaogopa. Wanahitaji kupewa moyo. Ikiwa mtu ni mzuri kwa mfano mshambuliaji au mlinzi ama beki, tunampa ushauri. Tunamshauri kutia bidii katika maeneo fulani fulani. Nguvu, mbinu, kasi na ukakamavu. Tunawapa ushauri kwa sababu sisi wenyewe tumepitia huko. Tunawaunga mkono kwa sababu tunataka kila wakiingia uwanjani wawe wanakumbuka yale wakubwa wao waliyowaambia. Wanaweza kufanikiwa ikiwa nia wanayo.

**Music**

12. **Narrator:**

Félix hakuwaza kuwa siku moja ataongoza kampuni. Alitaka kuwa mchezaji mpira wa kulipwa. Alivutiwa sana na wachezaji mpira wa Cameroon na mameneja aliowahi kukutana nao. Na hiyo ndio sababu kubwa iliyomfanya achague kazi yake mpya – kutambua kipaji kipya ambacho pengine huenda kikawavutia mashabiki. Hapo hapo anawaonya wachezaji mpira vijana wa Kiafrika ambao wana

ndoto ya kucheza mpira Ulaya kuwa safari hiyo ni ngumu - sio rahisi hata kidogo! Wengi kati ya mameneja binafsi ambao husafiri Afrika kutafuta vipaji vichanga ni sawa na wafanyabiashara haramu ya kuwauza watu. Wanatoa ahadi kubwa kubwa kwa vijana na wazazi wao. Lakini mara tu vijana hao wakifika kwenye nchi za kigeni mbali kabisa na nyumbani, wanajikuta wanatumbukia kwenye timu za daraja la tatu zisizojulikana katika miji midogo mbali sana na timu kama vile Real Madrid au Manchester United. Huko hawatambuliwi kama wachezaji wanaotarajiwa bali wanaajiriwa kwa ujira mdogo sana na mara nyingi wanateswa. Hayo ndio masikitiko aliyonayo Hzeina Félix, anasema ni hali ambayo wacheza mpira wengi wa Kiafrika watakubaliana nayo mara tu wafikapo katika nchi za kigeni.

**13. Voice clip Félix_5**

Haikuwa rahisi. Ni mkasa mkubwa Mwafrika anapojikuta katikati ya watu weupe – Nililazimika kupitia mazingira fulani ambayo hayakusaidia. Ilifikia wakati ambapo nilivunjika moyo sana. Nilitaka kuacha kila kitu lakini niliwaza kwa nini nifike kote huku halafu nibadili nia?" Niliona afadhali nivumilie tu kuweza kujenga uaminifu kwa wakufunzi ilinibidi nionyeshe umahiri kwenye timu na kujiwekea jina. Hivyo ndivyo nilivyofanya. Kulikuwa na wabaguzi wengi sana lakini mimi sikujali. Nilikuwa mpiganaji na lengo langu lilikuwa ni kufaulu. Hivyo ndivyo nilivyoweza kushinda vita.

14. **Narrator**:

Félix anasema iwapo unataka kucheza mpira, usisite hata kama ni vigumu. Mpira unaleta fedha za kutosha kuweza kubuni nafasi za ajira nchini mwake na kazi hiyo imemletea furaha kubwa maishani mwake, ndio maana siku ya Jumapili huenda uwanjani kuingalia klabu ya mpira ya chuo kikuu cha Ngaoundéré:

| | |
|---|---|
| **15.** | **Atmo_stadium** |

16. **Narrator:**

Félix anatambua jinsi vijana wanavyopenda kucheza mpira. Lakini anasikitika kuwa vijana wengi wanaacha masomo yao kwa ajili ya kucheza mpira. Anasema kwamba kufanya hivyo kunaathiri maisha yao ya baadae.

**17. Voice clip Félix_6**

Ningemwambia kijana yoyote anayetaka kucheza mpira kwamba afanye yote mawili acheze mpira na pia asome. Kwa sababu unahitaji elimu kabla ya kukabiliana na uwanja wa mpira. Ninasisitiza hili kwa sababu nafahamu. Nilitaka kuanza kucheza mpira nilipokuwa na miaka 18 na matumaini yangu yote yalikuwa kwenye mchezo huo.

| | |
|---|---|
| **18.** | **Atmo_television** |

19. **Narrator:**

Ni wakati sasa wakupata kinywaji katika baa ambayo inajulikana sana kwa sababu ya kuonyesha mechi za mpira pamoja na michezo mingine. Felix anatazama kwenye televisheni halafu anasema mara nyingine hujiwa na hamu ya kutaka kurudi Ulaya kwenye mashindano. Ingawaje kwa sasa anataka kubakia nyumbani na kuwasaidia watu wake. Anatoa mwito kwa waafrika wenzake walioko Ulaya wafuate nyayo zake.

**20. Felix's "final declaration"**

Ningemwambia kila mtu ambaye anamaliza mkataba wake wa kucheza mpira au mkataba wa kazi yoyote anayofanya, kwanza

ajifikirie mwenyewe halafu awafikirie wale wasio na kitu. – kuna wachezaji ambao hawajawahi kuhamia nchi za nje na pia hawana kazi. Hebu tujaribu kuwekeza fedha zetu kwenye biashara kama za nyumba na viwanja au kwenye kampuni zingine au hata kwenye ngome ili tupate shukurani kutoka kwa vijana ambao wanajitahidi kimaisha kwa kusema angalau namshukuru mtu yule kwa kuniwezesha kupata mkate wangu wa kila siku. Tujifikirie sisi wenyewe tukiwa Afrika!

**21. Atmo car starting up**

22. **Narrator:**

Kila siku baada ya kazi ngumu, Félix, ambaye ana watoto wawili, huingia ndani ya gari yake na kuelekea kwenye sehemu ya kufanyia mazoezi ya mwili ili kujitayarisha kwa siku nyingine inayofuata ya spoti na biashara.

**Music**

**23. Atmo : fade out to young footballers training in the background**

24. **Narrator:**

Wachezaji chipukizi wa kandanda mjini Ngaoundéré wana ombi moja tu – kupata fursa ya kucheza mpira katika timu za Ulaya halafu na wao wakirudi nyumbani wawekeze fedha zao kama vile Félix Hzeina. Farigou Oumarou ni mlinda lango “ goalkeeper” wa klabu ya chuo kikuu cha Ngaoundéré. Anavutiwa na yale aliyoyafanya Félix katika maisha yake:

25. **Son Fariqou Oumarou :**

Hzeina Félix ni mfano bora kwetu hapa Ngaoundéré. Nilipenda sana alivyocheza mpira. Hakuna mchezaji mwingine wa kulipwa anayewasaidia vijana kama yeye. Amenipa ushauri. Itakuwa vizuri kama mtu akipata fursa ya kwenda nje aige mfano wake.

**Music**

------------------------------------------------------------

**Outro:**

Asante kwa kusikiliza kipindi hiki katika makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Kwa kufahamu mengi zaidi, kusikiliza tena kipindi hiki au ukitaka kutuandikia maoni yako, tafadhali tembelea tovuti yetu. Anuani ni www.dw-world.de/lbe . Usisahau kujiunga nasi tena wakati ujao! Kwaheri kwa sasa.